MADA NA. 7 – Kukuza kuwalinda na kudumisha haki za makundi yaliyo hatarini na yenye mahitaji maalumu

***7.1 Wasilisho la Mada kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii* – Bw. Charwe**
Tanzania imeelekeza jitihada zake katika kujenga uchumi na kupunguza umasikini miongoni mwa raia wake kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi kwa kuimarisha huduma za jamii. Malengo matatu ya mwanzo ya MKUKUTA yote yanasisitiza umuhimu wa kujenga uwezo kiuchumi na kuboresha ustawi wa makundi maalum hususan Watu Wenye Ulemavu, Wazee na Wasiojiweza, Wanawake, Watoto na Vijana hasa Watoto Yatima na Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi.

Mifumo ya Kinga kwa Jamii (*social security fund*) husaidia baadhi ya watu katika jamii hasa wastaafu, lakini si kwa walemavu. Mpango Mkakati wa Taifa wa Sekta ya Afya wa tatu (2009) umeweka mkazo mkubwa wa kuimarisha Kinga ya Jamii kwa makundi maalum yaliyobainishwa hapo juu.

Haki za Makundi Maalumu:
- Lazima kuwe na mpango madhubuti kwa ajili ya makundi haya tete hasa kwa wale wenye ulemavu, mkazo ukiwa kwa watoto wenye ulemavu wawapo shuleni.
- Kushirikishwa kwenye maamuzi
- Haki ya kulindwa kwa maana ya kulindwa kisheria
- Ni wajibu wa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuendeleza jamii na haki za makundi maalumu.
- Serikali haiwajali watu hasa wale walioko kwenye uhitaji na makundi maalumu; asasi za kiraia zinajaribu kutoa msaada kwa makundi haya yakisaidiwa na sekta mbalimbali.
  Hitimisho: Kwa kuwa majanga na maafa yanayotokea mara kwa mara yanasababisha makundi maalum kuwa katika hali mbaya zaidi ya uhatarishi, serikali inao wajibu wa kuimarisha mifumo mbalimbali ya kinga ya jamii hasa ile ambayo itawajengea uwezo wa kujitegemea. Asasi za Kiraia hazina budi kuunga juhudi za serikali katika kuboresha mifumo hiyo pamoja na kubuni afua mbalimbali za kuendeleza vipaji vya wanajamii kutoka katika makundi maalum.

***7.2 Maoni kutoka CHAVITA* – Bw. Dickson Mveyenge**
Mkazo mkubwa uwe katika kinga ya jamii (*social protection*). Lugha ni chombo kikuu ambacho kinaunganisha watu wa jamii zote, k.m. Kiswahili. Lugha pia inaweza ikatenga watu. Je, washiriki tuliopo hapa tunafahamu matatizo wanayopata watu hawa hasa viziwi?

Mikakati ya kinga za jamii kwa viziwi:
- Kuwashirikisha wana-jamii ambao ni wazima, k.m. Polisi
- Viziwi washirikishwe katika mienendo yote ya jamii, kama vile mambo ya familia, shule za msingi na sekondari kwa viziwi, n.k.

- Wazazi wa viziwi wanatakiwa wawe watu wanaokubali tatizo la mtoto wao
- Vyombo vya habari vimeshindwa kutumia mbinu za kuwaelimisha viziwi , k.m. katika television, n.k.
- Mijadala mbalimbali inayoendelea katika Bunge, na Rasi haijaweza kuwafikia viziwi
- Ni vigumu kiziwi kupata huduma ya afya anapokuwa mgonjwa

***7.3 Mchango kutoka UWZ* – Bi. Talaa Saidi**

Nitazungumzia mambo ya viziwi na makundi maalumu huko Zanzibar. Zipo jumuiya nyingi zinafanya kazi huko Zanzibar lakini shughuli zao zimeathirika sana na mtikisiko wa uchumi. Serikali pia inajitahidi sana suala la walemavu. Usaidizi ni muhimu sana kwa mtu yoyote mwenye uhitaji.

Huduma za jamii:

- Afya – sera ya afya kwa walemavu, inawezekana kweli kwa mlemavu wa kawaida hasa wale waliopo vijijini?
- Elimu kwa viziwi
- Ajira kwa walemavu
- Mikopo kutoka taasisi za fedha, inawezekana kweli?
- Malezi, mavazi na lishe kwa walemavu. Bado hali ni mbaya mno ijapokuwa asasi za kiraia zinajitahidi lakini serikali imekaa kimya sana kuhusu masuala ya walemavu.
- Misaada ya kisheria – bado ni mdogo sana, hali bado ni mbaya.

Hitimisho: Kwa ujumla tusiache kupiga kelele kwa ajili ya haki za walemavu, tujitahidi kelele hizi zifike kwa walengwa, ambao ni serikali kuu na serikali za mitaa.

***7.4 Uzoefu kutoka DOLASED* – Bw. Gideon Kaino Mandesi**

Watu wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi katika jamii yenye mahitaji maalumu na wanastahili kulindwa na kupewa hifadhi kuanzia ngazi ya familia, jamii na serikali. Moja ya malengo ya MKUKUTA ni kuinua ubora wa hali ya maisha ya Watanzania, wakiwemo watu wenye ulemavu, kuwapa kinga ya jamii, kuhakikisha wanapata huduma ya afya, elimu, usafiri, ajira na kuhakikisha mazingira yanakuwa rafiki kwao.

Huduma za Jamii:

- Elimu – haki ya kupata elimu ni ya muhimu kwa kila mtu na hivyo mahitaji yao katika kupata elimu pamoja na usaidizi wanaostahili lazima yawekwe katika mfumo wa elimu ya jamii
- Ajira – walemavu wanao uwezo wa kuishi kwa kufanya kazi na wana nguvu ya kufanikisha kufanya kazi. Wanachohitaji katika jamii ni kuwezeshwa.
- Kinga ya jamii – hii ni muhimu sana kwa kundi hili. Watu wenye ulemavu ambao hawawezi kujipatia kipato na hawawezi kujiajiri kutokana na ulemavu wao ni vyema serikali kwa kushirikiana na wanajamii kuchukua hatua za kugharamia mahitaji yao ya kila siku kama chakula, mavazi na malazi (nyumba)

Hitimisho: Ulinzi wa jamii lazima uzingatie kwa kiwango kikubwa heshima na utu wa wanajamii waliopo katika makundi maalumu. Wasibaguliwe wala kuachwa bila kusaidiwa na familia, jamii na serikali.

7.5 Mjadala wa Pamoja, Maoni na Mapendekezo

Washiriki walikuwa na haya ya kuchangia katika mada hii:

- Suala la viziwi na walemavu, ni jinsi gani watapata haki zao za msingi?
- Utekelezaji wa misaada kwa walemavu ni mdogo sana hasa tukiongelea uwakilishi na ushiriki wao katika masuala ya maendeleo. Suala hili lipewe kipaumbele
- Tamko kwa jamii kwamba endapo kiziwi atafanya makosa basi apewe mkalimani awapo mbele ya vyombo vya sheria
- Kilio changu hasa ni kwa wazee walemavu waliopo vijijini, tunawasaidiaje hasa ukizingatia kwamba nao ni Watanzania.
- Sera yetu ya elimu kuhusu ulemavu bado haijamtendea haki mwanafunzi mlemavu, ambaye anaweza kufaulu lakini kutokana na unyanyapaa na kukosa fedha akashindwa kuendelea. Kwa hiyo serikali iliangalie hili la utendaji hasa ikisaidiana na asasi za kiraia
- Matatizo ni mengi sana kwa makundi haya, je jitihada zipo na zinafuatiliwa?
- Walemavu wawe kitu kimoja na matatizo yao yote yaende sehemu moja ukizingatia aina ya matatizo na mahitaji husika
- Walemavu tupate haki zetu na sio kutuambia tumepata msamaha wa kodi.
- Kuna walemavu wengi wamesahaulika, je, kuna mpango gani wa kuwasaidia hawa?
- Serikali haiwezi kufanya jambo bila kushinikizwa, kwa hiyo lazima tujue jinsi gani ya kuishinikiza hasa kwa matatizo ya makundi haya yanayoishi katika mazingira hatarishi.
- Walemavu waliolegea mwili mzima wanasaidiwaje kupata haki zao za msingi na mahitaji mengine?

Watoa mada walikuwa nao na mchango huu:

- Suala la ulemavu kwa wanawake ni gumu zaidi kutokana na wao wananyanyaswa sana, kuna masuala ya afya ya uzazi na wakina mama wengi wanahangaika na familia.

Hitimisho: Katibu Mkuu ameahidi kufanya marekebisho katika sekta hii ya walemavu kwa hiyo tuwe na subira hasa kwenye wizara hii ya Ustawi wa Jamii.